**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA WAZIRI MKUU**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# USIMAMIZI WA WATUMISHI KATIKA SERIKALI ZA MITAA

***Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Madiwani, Januari 2006)***

**JANUARI, 2006**

## USIMAMIZI WA WATUMISHI KATIKA SERIKALI ZA MITAA

***(Mada iliyoandaliwa kwa ajili ya Semina ya Madiwani, Januari 2006)***

### 1.0 Utangulizi

1.1 Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika Ibara ya 6 inafafanua neno "Serikali" kuwa ni pamoja na Serikali ya Jamhuri ya Muungano, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Serikali za Mitaa na pia mtu anayetekeleza madaraka au mamlaka yoyote kwa niaba ya Serikali yoyote.

Serikali za Mitaa ni vyombo vya kiutawala vya wananchi ambavyo kupitia vyombo hivyo wananchi wamepewa madaraka ya kuamua na kutekeleza shughuli zinazohusu maendeleo yao. Shughuli za Serikali za Mitaa ni:

(a) Kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa jumla.

(b) Kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa katika eneo lake;

(c) Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi; na

(d) Kuimarisha demokrasia katika eneo lake na kuitumia demokrasia kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Kama ilivyo kwa Serikali yoyote, Serikali za Mitaa zina uwezo wa kuajiri na kusimamia watumishi ambao ndio watendaji na watekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa. Na ili kuhakikisha kwamba pana uendeshaji mzuri wa Serikali za Mitaa, Sheria za Serikali za Mitaa Na. 7 na 8 za 1982 (Vifungu 117(1) na 53(1) kwa mfuatano) zimetoa uwezo kwa Serikali za Mitaa wa kutekeleza kazi na majukumu yake kwa **kutumia watumishi wake au wakala waliowateua rasmi.**

## 2.0 Utaratibu wa Kusimamia Watumishi Ulivyo Sasa

2.1 Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 pamoja na marekebisho yake (Sheria Na. 19 ya 2004) imetoa madaraka juu ya Usimamizi wa Watumishi wa Serikali za Mitaa kwa Mamlaka zifuatazo:

- Rais ndiye mamlaka ya uteuzi wa Wakurugenzi wa Jiji.

- Katibu Mkuu Kiongozi ni mamlaka ya kuthibitisha kazini na ya nidhamu kwa Wakurugenzi wa Jiji.

- Waziri mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa ni mamlaka ya uteuzi, kuthibitisha kazini, na nidhamu kwa Wakurugenzi Watendaji wa Wilaya, Wakurugenzi wa Miji, na Wakurugenzi wa Manispaa.

- Kila Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji ni mamlaka ya uteuzi, kuthibitisha kazini, kupandisha vyeo na nidhamu kwa watumishi ambao hawateuliwi na Rais au Waziri.

- Tume ya Utumishi wa Umma ina jukumu la kulinda misingi ya kuajiri watumishi wa Umma kwa kufuata sifa na ushindani.

- Wajibu mkubwa wa kuajiri, kuendeleza na kusimamia nidhamu ya watumishi utabaki mikononi mwa kila sehemu ya ajira. Kwa misingi hiyo, Halmashauri za Serikali za Mitaa ni Mamlaka kamili za Ajira za watumishi wake.

2.2 Ili kuhakikisha kuwa masuala ya utumishi yanasimamiwa ipasavyo, Mkurugenzi wa Halmashauri amepewa jukumu la siku hadi siku la kusimamia watumishi wote wanaofanya kazi katika Halmashauri yake.

2.3 Katika kila Halmashauri kuna Bodi ya Ajira ambayo ina majukumu ya kusimamia ajira katika Halmashauri husika. Majukumu ya Bodi za Ajira yameainishwa katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Majukumu hayo ni pamoja na kusaili na hatimaye kuwasilisha majina ya waliofaulu usaili kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

Mkurugenzi wa Halmashauri atawasilisha mapendekezo kwa Baraza la Halmashauri kwa uamuzi.

## 2.4 Uandaaji na Uidhinishaji wa Ikama za Halmashauri

Kila Halmashauri inalo jukumu la kupanga na kuimarisha mahitaji ya watumishi wake kulingana na shughuli zitakazotekelezwa na muundo wa Halmashauri husika. Zoezi hili linapaswa kufanyika kila mwaka kama sehemu ya uandaaji wa makisio ya mwaka ya Halmashauri. Kabla ya rasimu ya Makisio kuwasilishwa kwenye vikao vya Halmashauri na kuidhinishwa, inabidi Ikama ya Halmashauri iidhinishwe kwanza na Ofisi ya Rais, Menejimenti na Utumishi wa Umma.

## 2.5 Kutangaza Nafasi Zilizowazi

Utaratibu wa ajira katika Serikali za Mitaa umeainishwa katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2003. Nafasi zote zinazotakiwa kujazwa katika Halmashauri ni lazima zitangazwe ili kutoa nafasi ya ushindani. Matangazo hayo yatolewe kwa njia ya magazeti na pia yawekwe kwenye mbao za matangazo nje na ndani ya Halmashauri. Kwa nafasi ambazo Halmashauri ndiyo Mamlaka ya Uteuzi, Halmashauri itaiarifu Bodi ya Ajira ya Halmashauri ambayo, baada ya kushauriana na Tume ya Utumishi wa Umma, itatangaza nafasi husika. Kwa upande wa nafasi ya Mkurugenzi wa Halmashauri, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, baada ya kushauriana na Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa ataiarifu Tume ya Utumishi wa Umma na Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu kuwepo kwa nafasi hiyo. Baada ya kupokea taarifa hiyo, Tume ya Utumishi wa Umma itatangaza nafasi hiyo kwa kufuata utaratibu uliokwishaelezwa hapo juu.

## 2.6 Utaratibu wa Usaili

2.6.1 Usaili wa wagombea nafasi ya Mkurugenzi wa Halmashauri hufanywa na Tume ya Utumishi wa Umma.

2.6.2 Inapotokea nafasi wazi ambayo Mamlaka ya Uteuzi ili kuijaza ni Halmashauri, Halmashauri itaiarifu Bodi ya Ajira ya Halmashauri kuhusu kuwepo kwa nafasi hiyo ambayo Bodi itatangaza na kisha

itasaili waombaji na kuwasilisha kwa Halmashauri husika orodha ya waombaji.

## 2.7 Taratibu za Uteuzi

2.7.1 Iwapo nafasi ya kujazwa ni ya Mkurugenzi wa Halmashauri, Tume ya Utumishi wa Umma baada ya kuwasaili waombaji itawasilisha orodha ya waombaji wenye sifa za kufikiriwa kujaza nafasi hiyo kwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ambaye ataifikisha kwa Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa kwa uteuzi, baada ya kushauriana na Halmashauri husika.

2.7.2 Kwa nafasi ambazo Mamlaka ya Uteuzi ni Halmashauri yenyewe, baada ya kukamilisha shughuli za usaili, Bodi ya Ajira itawasilisha kwa Halmashauri husika majina ya waombaji wanaostahili kuajiriwa kufuatana na stahili zao, na Halmashauri itafanya uteuzi kulingana na idadi ya watumishi wanaotakiwa.

## 2.8 Taratibu za Kuajiri

Baada ya Waziri kufanya uteuzi wa Mkurugenzi wa Halmashauri husika, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mkono wake, atamwandikia Mkurugenzi aliyeteuliwa barua ya ajira, na kuinakili kwa Mwenyekiti/Meya wa Halmashauri husika. Kwa watumishi wengine wa Halmashauri, Mkurugenzi wa Halmashauri, kwa mkono wake, atamwandikia mtumishi aliyeteuliwa barua ya ajira kufuatana na uteuzi wa Halmashauri.

# 3.0 Malipo ya Mshahara

3.1 Halmashauri ndiyo Mwajiri wa watumishi wa Umma walio kwenye Serikali za Mitaa, na kama Mwajiri inawajibika kikamilifu na malipo ya mishahara ya Watumishi hata pale ambapo mishahara hiyo inatokana na Ruzuku kutoka Serikali Kuu.

3.1.2 Viwango vya mishahara ya watumishi wa Umma walio katika Serikali za Mitaa hupangwa na Serikali Kuu kupitia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Halmashauri zinatakiwa kuhakikisha kuwa Makisio ya gharama za mishahara yamezingatia ikama iliyoidhinishwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, kabla ya kupitisha Makisio ya kila mwaka. Jukumu lingine la Halmashauri ni

kuweka utaratibu wa ulipaji wa mishahara ambao hauleti usumbufu kwa watumishi na unaowahakikishia malipo ya mishahara yao ndani ya muda unaotakiwa. Kwa sasa Serikali imeweka utaratibu wa kulipa mishahara ya Watumishi kupitia benki. Wakurugenzi, kama Maafisa Wahasibu, wanapaswa kusimamia kwa karibu sana utayarishaji na ulipaji wa mishahara katika Halmashauri zao ili kuondoa kabisa **watumishi hewa** kwenye orodha ya mishahara (Payroll) Serikalini. Wakurugenzi wote wazingatie maelekezo waliyopewa na wataalamu wa fedha katika Timu za Kanda na namna ya kugundua malipo ya mishahara yenye uwezekano wa kuwa na watumishi hewa.

## 4.0 Uendelezaji wa Watumishi

4.1 Ni jukumu la kila Halmashauri kuwapatia mafunzo na kuwaendeleza watumishi wake. Katika kufanikisha jukumu hili, Mamlaka za Serikali za Mitaa zitasaidiwa na kuungwa mkono na Wizara za Sekta zinazohusika, vyama vya kitaalamu, na taasisi mbalimbali zinazohusika na utoaji mafunzo.

4.1.1 Kila Mamlaka ya Serikali za Mitaa itatakiwa kuandaa mpango wa maendeleo ya watumishi ambao utazingatia ushauri wa Wizara za kisekta kuhusu aina ya mafunzo yanayotakiwa kwa watumishi wa sekta husika na sifa za kitaalamu zinazohitajika katika madaraja mbalimbali ya watumishi wa Serikali za Mitaa na kuhakikisha kwamba fedha inatengwa katika makisio kwa ajili ya mafunzo na maendeleo ya watumishi wa Halmashauri. Ni muhimu baadhi ya Madiwani katika baadhi ya Halmashauri wasiotaka watumishi, hasa wasiotoka katika eneo la Halmashauri, kugharamiwa na Halmashauri zao waache ubaguzi wa aina hiyo kwa sababu msimamo wa aina hiyo ni kinyume na Katiba ya Jamhuri na Sera za nchi yetu.

4.1.2 Ofisi ya Rais – Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, baada ya kushauriana na wizara za kisekta, itaandaa programu ya mafunzo na maendeleo ya watumishi kitaifa kwa ajili ya watumishi wataalamu wanaofanya kazi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, na kuhakikisha kwamba juhudi zinafanywa ili watumishi hao waweze kujumuishwa katika mipango ya mafunzo ya wizara za sekta zinazohusika.

**Kupandishwa Vyeo Watumishi wa Umma walio kwenye Serikali za Mitaa**

4.1.3 Mamlaka ya kupandisha cheo Wakurugenzi wa Halmashauri ni Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa isipokuwa kwa Mkurugenzi wa Jiji ambaye mamlaka yake ya kumpandisha cheo ni Rais.

4.1.4 Kwa watumishi wengine, Halmashauri ndiyo yenye mamlaka juu ya mambo yote yanayohusu upandishwaji vyeo wa watumishi hao.

4.1.5 Mkurugenzi wa Halmashauri baada ya kuzingatia muundo wa utumishi wa Halmashauri atatayarisha orodha ya watumishi wanaostahili kupandishwa vyeo na kuwasilisha majina hayo kwa Halmashauri kwa ajili ya kujadiliwa na kufanyiwa maamuzi.

4.1.6 Upandishwaji vyeo utazingatia stahili, ufanisi na uthabiti katika utendaji kazi, tathmini ya utendaji kazi ya wazi (OPRAS), sifa za kielimu, ujuzi, uadilifu na sifa binafsi za mhusika.

## 5.0 Uhamisho wa Watumishi

5.1.1 Mojawapo ya matokeo ya utekelezaji wa Sera ya Upelekaji wa Madaraka kwa Wananchi ni kuanzishwa kwa mahusiano ya kawaida ya Mwajiri na Mwajiriwa kati ya Halmashauri na Watumishi wa Umma walio katika Serikali za Mitaa, na kutenganisha uhusiano uliokuwepo awali kati ya Watumishi wa Kisekta walio katika Serikali za Mitaa na Wizara za Sekta husika. Hii ina maana ya kwamba kwa kawaida mtumishi wa Halmashauri anatarajiwa kubaki katika utumishi wa Halmashauri inayomwajiri kulingana na masharti ya utumishi wake katika Halmashauri hiyo. Kwa ajili ya kuboresha ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi, watumishi wa Umma walio katika Serikali za Mitaa wanaweza kuhamishwa kutoka Halmashauri moja kwenda Halmashauri nyingine kwa kuzingatia utaratibu maalumu. Mfano ufuatao utasaidia kuelezea suala hili: mtumishi katika Halmashauri moja anaruhusiwa kuomba nafasi wazi ambayo imetangazwa na baada ya usaili akishinda na kuteuliwa anahamia huko kwenda kujaza nafasi husika. Mtumishi huyo atahesabiwa kuwa amehamishiwa katika Halmashauri ambako uteuzi umefanyika ili kulinda utumishi wake wa nyuma. Uhamisho wa mtumishi yeyote katika Serikali za Mitaa ni lazima upate kibali cha Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais,

Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Hata hivyo, mtumishi hatahamishwa kushika nafasi ya utumishi wenye masharti tofauti na utumishi wake bila ridhaa yake.

5.1.2 Uhamisho ndani ya Halmashauri, kutoka kituo kimoja kwenda kituo kingine cha kazi, utazingatia misingi ya kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma na, kamwe, hautakiwi kufanywa kama hatua ya **kinidhamu**, ambayo inatakiwa ichukuliwe na kutekelezwa pale mtumishi alipo. Utaratibu huu utasaidia kuondoa gharama zisizokuwa za lazima ambazo Halmashauri hubebeshwa kutokana na baadhi ya Madiwani, ambao wakishakorofishana na baadhi ya watendaji katika Kata zao (mara nyingine kutokana na sababu za binafsi), humshinikiza Mkurugenzi awahamishe na hivyo kuiingiza Halmashauri katika hasara !

## 6.0 Usimamiaji wa Nidhamu ya Watumishi katika Serikali za Mitaa

6.1.1 Halmashauri zimepewa uwezo na jukumu la kusimamia nidhamu ya watumishi wa Umma walio katika Utumishi wa Serikali za Mitaa. Kwa upande wa Wakurugenzi wa Jiji, Katibu Mkuu Kiongozi ndiye Mamlaka ya Nidhamu na kwa Wakurugenzi wengine wote Waziri Mwenye Dhamana ya Serikali za Mitaa ndiye Mamlaka ya Nidhamu. Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji ni mamlaka ya nidhamu kwa watumishi wake ambao si Wakurugenzi.

6.1.2 Masuala ya nidhamu ya watumishi wa Halmashauri yatajadiliwa kwanza na kutolewa mapendekezo na Kamati ya Fedha na Uongozi/Fedha, Uongozi na Mipango kabla ya kuwasilishwa kwenye Halmashauri kwa uamuzi wa mwisho. Ieleweke kuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ndiye ataanzisha na kuendeleza mchakato wote wa masuala ya nidhamu ili kuhakikisha kuwa taratibu zinazingatiwa kikamilifu. **Kamwe Mheshimiwa Diwani au Meya/Mwenyekiti wa Halmashauri peke yake hawezi kuanzisha hatua za nidhamu bila kupitia kwa Mkurugenzi**. Uamuzi wa mwisho wa kutoa adhabu katika kesi za nidhamu utatolewa katika **kikao halali cha Halmashauri.**

6.1.3 Lengo kuu la kuzipa Halmashauri uwezo wa kusimamia nidhamu ya watumishi wao ni kuhakikisha kuwa watumishi hao wanafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na taratibu zilizowekwa na wanatoa

huduma kwa wananchi kwa uaminifu na uadilifu wa kiwango cha hali ya juu ili kuboresha utoaji wa huduma muhimu kwa wananchi. Vile - vile uwezo huu wa Halmashauri unaweka msingi imara wa **uwajibikaji** wa watumishi kwenye mamlaka zilizowaajiri.

6.1.4 Katika kusimamia nidhamu ya watumishi, Halmashauri zitatakiwa kuzingatia misingi ya haki, ukweli, na maslahi ya umma na kuwapa wale wanaotuhumiwa kwa vitendo vya utovu wa nidhamu fursa ya kusikilizwa na kujitetea kabla ya uamuzi kufanywa.

6.1.5 Kama walivyo wananchi wengine, watumishi wa Umma walio kwenye Serikali za Mitaa wana haki za msingi na pia haki zinazoendana na utumishi wao ambazo lazima zithaminiwe, zilindwe na kuzingatiwa wakati wote na Halmashauri zinazowaajiri. Vitisho, uonevu, na ukandamizaji lazima viepukwe ili kuwajengea watumishi wa umma walio katika Serikali za Mitaa mazingira yatakayowawezesha kuongeza ufanisi na tija katika utendaji wao.

6.1.6 **Rufaa**

Pale ambapo mtumishi wa Serikali za Mitaa haridhiki na adhabu ya kinidhamu aliyopewa na Halmashauri, mtumishi huyo atakata rufaa kwenye Tume ya Utumishi wa Umma na iwapo hataridhika na uamuzi wa Tume, atakata rufaa kwa Rais, ambaye uamuzi wake utakuwa ni wa mwisho.

6.1.7 Taratibu za kushughulikia masuala ya nidhamu ya watumishi walio katika ngazi za kawaida (Operational Service) zitakuwa kama ilivyoelekezwa katika Sheria ya Usalama Kazini ya 1964.

## 7.0 Motisha kwa Watumishi Wanaofanya kazi katika Serikali za Mitaa

7.1 Halmashauri zote nchini zimeshauriwa na zinaendelea kushauriwa kubuni na kuweka utaratibu ulio wazi na endelevu wa kutoa motisha mbalimbali kwa watumishi wake. Motisha hizo zinaweza kuwa za fedha au aina nyinginezo ambazo sio fedha. Lengo kuu ni kujaribu kuwavutia watumishi waajiriwe na kubakia katika utumishi wa Serikali za Mitaa.

Mpaka sasa zipo Halmashauri chache ambazo zimeonesha mfano bora wa kutoa motisha mbalimbali kwa watumishi wake. Mifano ya Halmashauri hizo imeoneshwa katika Jedwali Na. 1 hapa chini:

**JEDWALI NA. 1: MOTISHA KWA WATUMISHI**

| KANDA | HALMASHAURI | AINA ZA MOTISHA |
|---|---|---|
| 1. DODOMA | (i) Mpwapwa DC | Ilitoa pikipiki 18 kwa Maafisa Watendaji wa Kata |
| | (ii) Kasulu DC | Ilitoa motisha kwa njia ya kuwadhamini watumishi wake (2) kupatiwa mikopo kutoka Benki ya (NMB) kwa ajili ya kununulia mashine mbili (2) za kusaga unga |
| 2. MBEYA | Mbinga DC | • Maafisa Watendaji wa Kata 21 walipewa Baiskeli<br>• Wakuu wa Idara walipewa pikipiki<br>• Wahudumu wa Afya – Health Attendants 60 walipewa baiskeli |
| 3. MTWARA | Masasi DC | • Maafisa wapya wanaoajiriwa na Halmashauri ambao viwango vyao vya mishahara viko kati ya TGS – D na kuendelea TZS. 139,430/= – 173,750/= hupewa posho ya nyumba (Housing Allowance)<br>• Watumishi wa Halmashauri wanaoamua kujijengea nyumba zao za kuishi palepale Masasi Wilayani – wanapewa usafiri wa vifaa vya ujenzi<br>• Wakuu wa Idara wanapewa TZS. 50,000/= kila mwezi kwa ajili ya matumizi ya simu za mikononi |

| KANDA | HALMASHAURI | AINA ZA MOTISHA |
|---|---|---|
| 4. MWANZA | Kahama DC | Halmashauri ilitumia fedha zake yenyewe kuwasomesha watumishi wake kama ifuatavyo:<br><br>• Afisa Ugavi mmoja (1) masomo ya Stashahada<br><br>• Afisa Kilimo Msaidizi – 1 – masomo ya Stashahada miaka mitatu (3) katika Chuo cha Sokoine cha Kilimo<br><br>• Afisa Biashara 1 – masomo ya MBA ya miaka miwili (2) Chuo Kikuu Mzumbe |

7.2 Hizi ni baadhi tu ya Halmashauri chache ambazo zimetoa motisha kwa watumishi wake. Halmashauri nyingine nazo zinashauriwa na kuhimizwa kuiga mifano bora, kutoka kwa wenzao, ya kutoa motisha kwa watumishi wao.

## 8.0 HITIMISHO

Kama ilivyokwishaelezwa hapo awali, ni kwamba hivi sasa tumo katika mwaka wa sita wa kutekeleza Mpango wa Uboreshaji wa Mfumo wa Serikali za Mitaa. Hivyo, Serikali inategemea kwamba kadiri miaka inavyopita ndivyo Madiwani wanavyopaswa kuzingatia kanuni za msingi za usimamizi wa watumishi wa Umma.

Ili Mheshimiwa Diwani, kama kiongozi na mhamasishaji wa shughuli za maendeleo katika eneo lake, aweze kutekeleza wajibu wake ipasavyo ni muhimu afahamu kwa upeo mkubwa mahusiano yake kiutendaji na watumishi katika Halmashauri yake. Kwa kuzingatia umuhimu huo na kwa kuzingatia kwamba Madiwani ni kati ya viongozi muhimu walio karibu sana na wananchi, na wanatekeleza majukumu yao kwa kushirikiana na watumishi walio katika Halmashauri zao, Madiwani hawana budi kusimamia watumishi katika Serikali za Mitaa kwa mujibu wa sheria ili kutenda haki. Ikumbukwe

kwamba watumishi ni mojawapo ya **rasilimali muhimu** inayohitajika katika **kubuni**, **kupanga** na **kutekeleza** majukumu ya Halmashauri kwa lengo la kuinua kiwango cha utoaji huduma bora kwa wananchi na hatimaye kuondoa umaskini uliokithiri miongoni mwa Watanzania.

__________xxx_________